



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MADINI

SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CB. 27/404/01/7

20 Januari, 2023

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA,

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) litauza vifaa chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara. Vifaa hivyo ni pamoja na Gari (Lori) moja, samani za ofisi, mashine / mitambo mbalimbali za utafutaji na uchimbaji madini na vifaa vya ofisi. Vifaa hivi vitauzwa **tarehe 08 Februari, 2023** kuanzia **saa 4:00** asubuhi katika ofisi za Shirika zilizopo Barabara ya Mirembe, Hazina, Kitalu Na. 173, Block "W" Dodoma.

MASHARTI YA MNADA

1. Kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa **asilimia 25** ya thamani ya kifaa atakachokinunua siku hiyo hiyo ya mnada na fedha zitakazobaki zitalipwa ndani ya **siku saba (7)**.
3. Mnunuzi atachukua / kuondoa vifaa vyake ndani ya siku **saba (7)** baada ya mnada.
4. Ruhusa ya kuangalia / kukagua vifaa itatolewa **siku mbili (2)** kabla ya tarehe ya kufanyika kwa mnada kuanzia **saa 3:00 asubuhi** hadi **saa 10:00 jioni**.

Imetolewa na:

Dkt. Venance B. Mwasse
MKURUGENZI MTENDAJI

Nakala: Msimamizi wa Mali za Serikali (M),
S. L.P 230,
DODOMA.